

Umuhimu wa wanawake kwenye miradi ya viazi lische



Viazi lische vinaweza kuchangia katika malengo ya maendeleo na kuwawezesha wanawake



- Akina mama wakiwa kifua mbele katika kuhamasisha matumizi Viazi lische (picha na Marie-Josse)

Viazi lische ni zao lenye matumizi mbalimbali ambalo licha ya kuchangia usalama wa chakula na lische pia linachangia kuboresha upatikanaji wa chakula na kipato pindi wakulima wanapozalisha aina zenye mavuno mengi kwa kufuata mbinu shirikishi za udhibiti wa visumbufu pamoja na kuongeza thamani. Kwa nini miradi ya viazi lische ilenge zaidi wanawake wakati inaweza kuboresha usalama wa chakula na lische kwa wote?

Jibu ni rahisi: Sababu kubwa ni kuwa wanawake ni muhimu katika suala la usalama wa chakula na lische katika ngazi ya kaya na pia wanatoa mchango mkubwa katika ustawi na faida ya kaya nzima. Kuwekeza katika wanawake kama watoa huduma, wakulima, wasindikaji na watu wenye kipato ndipo viazi

lische vinapoweza kuchangia katika lische na uchumi katika ngazi ya kaya na ya Taifa.

✦ Kuimarisha nafasi ya mwanamke katika utoaji wa maamuzi juu ya lische:

Wanawake waishio nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ndio watoa maamuzi ya chakula cha mtoto na lische ya kaya. Kuhimiza viazi lische kunagusa masuala ya elimu, kuboresha ufahamu wa lische, kilimo na kutoa maamuzi. Yote hayo yanakuwa chanzo cha mabadiliko ya lische na pia ni njia ya kuwawezesha wanawake kupitia vikundi, mafunzo ya kusoma na kuandika, na njia nyinginezo. Kwa kupitia njia hiyo ya uwezeshaji, lische na mbinu nyinginezo zinaimarisha majukumu ya wanawake katika lische badala ya kuwaangalia wanawake kama njia ya kuboresha lische ya mtoto tu. Pia ni muhimu kuhamasisha wanaume kuchukua jukumu lao la lische ya kaya na usalama wa chakula sawa na wanawake.

✦ Kuwajengea Uwezo akina mama kama wazalishaji

Kuwawezesha wanawake kuwa wazalishaji: Katika nchi nyingi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara viazi vitamu huzalishwa kiasili, huuzwa na kusindikwa kwa kiwango kidogo na wanawake. Hiyo hutokana na wanawake kukosa rasilimali za kusaidia uzalishaji kama vile teknolojia, ardhi, nguvu kazi, elimu na huduma za kifedha. Kutokana na wanawake kutoweza kufanya maamuzi katika kaya huchangia mazao ya viazi lische kuwa kwa kiwango kidogo. Uanzishaji wa aina za viazi lische zitoazo mavuno mengi kwa wakulima wanawake kwa uzalishaji kwenye bustani au kwenye mashamba na kutoa ushauri juu ya kuboresha uzalishaji na upatikanaji wa pembejeo kunatoa fursa ya kuongeza uzalishaji wenye tija kwa wanawake.



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



■ Biashara kandokando ya barabara nchini Zambia (Picha na J. Low)

Ongezeko hilo linaweza kupunguza tatizo la upungufu wa vitamini A na kuboresha usalama wa chakula kutokana na wanawake kutumia viazi lishe zaidi ya wanaume kwa chakula cha watoto na matumizi ya kaya. Mbinu ya uboreshaji wa bustani ndogondogo itatumika kama chanzo cha shughuli za kuwawezesha wanawake kama vile kupata ushauri, elimu na mafunzo ya kuhesabu, na kujengea uwezo ili wawe wataalamu wa viazi lishe katika jamii yao. Mbinu hiyo pia lazima iende sambamba na jitihada za kuboresha lishe kwa ujumla.

Hata hivyo, katika maeneo ambayo wanaume hupanda viazi vitamu au wanajihusisha na uzalishaji wa zao hilo kutokana na ongezeko la soko, ni muhimu kusaidia shughuli za uzalishaji wa jinsia zote mbili ili wanawake wasiishie kuzalisha viazi lishe kwa matumizi ya kaya lakini wapate fursa sawa na wanaume ya kushiriki katika uzalishaji wa kibiashara. Teknolojia, mafunzo na huduma zinazohusiana na viazi lishe ni lazima ziguse masuala ya kijinsia na uwajibikaji. Mikakati hiyo huwa chanzo cha mafunzo ya kujenga uwezo kwa ajili ya uwezesaji wa wanawake, elimu na mabadiliko ya kitabia. Soko la viazi lishe linavyozidi kuongezeka, inabidi kuhimiza mikakati ya kijinsia katika kaya kama vile mafunzo kwa wanaume na wanawake katika kupanga usalama wa chakula na utoaji wa maamuzi katika ngazi ya kaya ili kuhakikisha mavuno ya kutosha yanatengwa kukidhi matumizi ya kaya na sehemu nyingine mahususi kwa kipato kinachotakiwa kugawanywa sawa ndani ya kaya.

❖ **Kuwainua wanawake kwa kipato.** Inafahamika kwamba wanawake wakiwa na kipato cha ziada, kipato hicho hutumika kwenye chakula, mavazi, afya, na elimu ya watoto wao kuliko kipato cha ziada cha wanaume. Kipato cha ziada huwaongeza wanawake nguvu ya kutoa maamuzi ndani ya kaya, kitu ambacho kinachangia katika lishe, afya na elimu ya watoto, hali bora na mafanikio ya binafsi kwa wanawake wenyewe.

Mavuno ya kutosha ya viazi lishe yatawawezesha wanawake kuuza na kusindika viazi lishe. Kuna haja ya kubuni usawa wa kijinsia katika shughuli za kibiashara ili kuhakikisha wanawake hawabaki nyuma katika uzalishaji na usindikaji wa viazi lishe. Ili kuhakikisha kwamba wanawake wana fursa sawa na wanaume katika ngazi zote za uzalishaji wa viazi lishe basi mafunzo ya ujasiri-amali, huduma za fedha na rasilimali nyingine ni lazima yazingatie usawa wa kijinsia.

Kuhakikisha kwamba mahitaji na maslahi ya wanawake yanazingatiwa katika uzalishaji, usindikaji na masoko kutaongeza ufanisi wa mfumo wa kilimo na chakula, na wakati huo huo kusaidia malengo ya usawa wa kijinsia.

Kwa kupitia mbinu ya uwezesaji, viazi lishe vinaweza kuchangia kuboresha haki za wanawake na malengo ya maendeleo ya Taifa.

Mradi wa Kuwafikia Mawakala wa Mabadiliko unasisitiza uwekezaji katika viazi lishe kama mbinu ya kupambana na upungufu wa vitamini A miongoni mwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na mama zao. Mabadiliko hayo pia yanalenga kujenga uwezo wa taasisi kubuni na kutekeleza miradi ya kijinsia ili kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya viazi lishe katika nchi chache Afrika. Juhudi zake zinachangia kukuza mpango wa viazi lishe kwa afya na kipato ambao unalenga kuboresha maisha ya familia milioni 10 za Afrika ifikapo mwaka 2020.

Mawasiliano:

Adiel Mbabu (CIP)
Meneja Mradi
Baruapepe:a.mbabu@cgiar.org

Sonii David (HKI)
Mhamasishaji na Mshauri wa Jinsia
sdavid@hki.org

Jan Low
Mkuu wa Mradi
Baruapepe:j.low@cgiar.org